# Takwimu za Ulemavu Shuleni: Majaribio ya Moduli ya Kukadiri Uwezo wa Mtoto – Toleo (Nakala ya) la Mwalimu (CFM-TV) katika Hali za Dharura na Hatari/ Migogoro za Muda Mrefu

Tafiti za Muhtasari

wa RS | Nambari 45 | Waandishi Aude Brus, Sandrine Bohan-Jacquot, Yahoko Asai
3I Kitengo cha / Idara ya Ustadi wa Ujumuishaji wa Kijamii / Mradi wa Eneo la Afrika Mashariki
2023

## Kuhusu HI

Humanity & Inclusion (HI) hufanya kazi na watu walio na ulemavu na jamii hafifu zilizo kwenye mazingira magumu. HI huwa mtetezi ili kushughulikia mahitaji yao muhimu, kuboresha hali zao za maisha, na kuendeleza heshima kwa utu wao pamoja na haki zao za kimsingi. HI huchangia katika mazungumzo ya kimataifa kuhusu takwimu zinazozingatia na kuainisha ulemavu.

## Kuhusu muhtasari huu

Chapisho la Humanity & Inclusion

## Kuhusu utafiti huu

Utafiti huu umefanyika kwa ushirikiano na Kikundi cha Washington cha takwimu za ulemavu. Shukrani pia kwa msaada wa kifedha kutoka kwa Education Cannot Wait.

## A. Muktadha wa utafiti

Takwimu ni muhimu sana katika kukabiliana na changamoto za kijamii na kuhakikisha kwamba watu walio na ulemavu 'hawabaki nyuma'. Ingawa Ripoti ya Dunia ya Ulemavu inakadiria kuwa hadi 15% ya idadi ya watu wana ulemavu, ukusanyaji wa takwimu sahihi za ulemavu bado ni changamoto. Mara nyingi ni ghali na si sahihi. Pengo hili la takwimu linatatanisha haswa kwa watoto na vijana walio na ulemavu, kwa kuwafanya "wasiweze kuonekana kisiasa na kijamii," na kuweka vizuizi kwa hao kufikia na kupata huduma muhimu kama elimu na afya.

'Short Set (SS) of the Washington Group on Disability Statistics' hutumika sana kukusanya takwimu za ulemavu kwa watu wazima. Hata hivyo, SS bado ina mapungufu inapotumika kwa watoto. Kama suluhisho la changamoto za SS ikitumika kwa watoto, UNICEF iliunda Moduli ya Kukadiri Utendaji/ Uwezo wa Mtoto (CFM) inayolenga kutambulisha watoto wenye matatizo ya utendaji yanayoweza kuzuia kushiriki kwao katika shughuli za kila siku. Walezi wa karibu ndio hujibu maswali kama wawakilishi. Kujibu kwa maswali ya SS yanaweza kufanywa katika maeneo mbalimbali, Kwa ufanisi zaidi nyumbani panafaa Zaidi lakini pia hata shuleni. Hata hivyo, maswali 24 ni mengi sana yakujibiwa na wazazi wanapoitwa mashuleni kuhusu kila mtoto wao aliyesajiliwa shuleni, hasa katika hali za dharura na migogoro inayochukua muda mrefu.



Hivyo, Moduli ya Utendaji wa Mtoto - Toleo la Mwalimu (CFM-TV) iliundwa na inaruhusu walimu kuwa wawakilishi. Ina maswali 13 ya utendaji tofauti tofauti, kuwezesha walimu kutathmini matatizo ya utendaji wa wanafunzi wao.

HI ilitafiti ufanisi, uaminifu, na matokeo ya elimu jumuishi wa CFM-TV katika muktadha wa changamoto katika makazi ya wakimbizi ya Kyaka II nchini Uganda.


## B. Malengo ya Jumla na Mahususi

Mradi wa Disability Data in School (DiDa) (Takwimu za Ulemavu Shuleni) unalenga kuchangia kupeana takwimu  sahihi  kuhusu ulemavu shuleni katika muktadha wa mazingira hatari. Lengo kuu la kwanza la utafiti huu,  lilikuwa kutathmini kueleweka kwa CFM-TV kwa wahojiwa walengwa. Lengo kuu la pili lilikuwa kutathmini iwapo CFM-TV itatoa takwimu thabiti Mradi unachunguza uthabiti wa matokeo wakati yanaporudiwa kwa hali zinazofanana (walimu wale wale wakitathmini wanafunzi wale wale baada ya muda wawa wiki tatu) na kiwango ambacho matokeo haya yataafikiana na njia zingine za ukusanyaji wa takwimu na wahojiwa wengine (CFM ya walezi na matokeo ya watoto wenyewe kujijibia wenye umri kati ya miaka 12-17). La mwisho, utafiti unalenga kutathmini uwezekano wa utekelezaji wa CFM-TV katika hali halisi za shule/darasa.

## C. Mbinu za Utafiti

Utafiti huu unatumia mbinu mchanganyiko. Mwanzo, mahojiano ya uelewaji wa akili yalifanywa kwa walimu na wanafunzi wenye umri wa zaidi ya miaka 12 katika shule mbili zilizochaguliwa  bila kutumia taratibu zozote. Ili kuchunguza uthabiti wa CFM-TV, shule tatu zingine zilichaguliwa bila kutumia taratibu zozote.na darasa moja kwa kila daraja lilichaguliwa  katika kila shule. Kwa ujumla zikawa madarasa 21 na huku  walimu wakiwa 21. Utafiti wa kupeana ripoti kwa idadi uliendeshwa kupitia makundi matatu: walimu (vipindi viwili, kila baada ya muda wa wiki tatu), walezi, na wanafunzi wenye umri wa zaidi ya miaka 12. Hatimaye, majadiliano ya kikundi kwa vikundi vitatu na uchunguzi wa kesi tano maalum zilifanywa ili kutathmini uwezekano wa kutekeleza CFM-TV katika mazingira mengine ya shule. Mchoro ufuatao unaonyesha muundo wa utafiti.

**Takwimu: Uwasilishaji wa mbinu ya utafiti na watu walengwa.**




## D. Matokeo

### (1) Ufahamu wa CFM-TV kwa walimu

Kwa ujumla, walimu walichukulia maswali ya CFM-TV vyema huku wakiyataja kuwa 'rahisi kwa walengwa kutumia' na yanafaa kulingana na mazingira yao ya kazi. Ingawaje, tofauti iliibuka kwenye maswali: baadhi ya maswali ya utendaji/ uwezo hayakuzua ugumu wowote (au kidogo) (kwa mfano, kujibu maswali kuhusu uwezo wa kuona, kusikia, kutembea). Swali la 'kukumbuka' badala ya uwezo wa kuweka kwenye kumbukizi, walimu walizingatia uwezo wa wanafunzi kukumbuka masomo waliyoyasoma jana yake. Pia baadhi ya walimu walishangazwa na swali la 'kupata marafiki', kwani hawakudhani ni jukumu au hoja ya mwalimu kuzingatia. Matokeo ya utafiti huu yalitumika kuboresha mafunzo ya walimu.

### (2) Uthabiti wa CFM-TV

- Uthabiti wa Mtafiti Mmoja wa CFM-TV kwa takwimu ulifanywa kwa kulinganisha uwiano wa idadi ya wanafunzi wenye vikwazo katika utendaji wao walipotathminiwa na walimu katika wakati tofauti, kila baada ya wiki tatu. Matokeo yalionyesha kiwango cha makubaliano ambayo ni wastani, kuashiria kiwango cha wastani cha uthabiti katika kutathmini hali ya ulemavu kwa wanafunzi wa darasa lao.

- Uthabiti wa Wataalamu Wawili wa takwimu hizo ulifanywa kwa kulinganisha tathmini za kwanza za walimu na walezi, kisha kwa kulinganisha tathmini za walimu na zile Watoto wenyewe walijijibia (Kwa watoto kati ya miaka 12 na 17).

## Matokeo ya Walimu yakilinganishwa na yale ya Walezi:

Matokeo yanaonyesha kwamba walezi walitambua watoto wengi zaidi wenye ugumu kwenye utendaji ikilinganishwa na walimu. Walezi na walimu walitathmini asilimia sawa kuhusu vipimo vya kumbukumbu, na matokeo ya kudhibiti tabia yakawa yanakaribiana sana. Hata hivyo, tofauti kubwa zilionekana katika vipimo vingine vya utendaji/uwezo.

Uchambuzi wa makubaliano kati ya walimu na walezi kuhusu hali ya ulemavu wa watoto yalizua matokeo ya kuvutia. Matokeo yaliashiria kuwa kuna uwiano kiasi kati ya majibu ya walimu na yale ya walezi katika tathmini zao za hali ya ulemavu katika vipimo vyote vya utendaji. Hata hivyo, licha ya ukosefu wa uhusiano na uwiano madhubuti, inavutia kwamba walimu na walezi walikubaliana kuhusu kutokuwepo kwa shida yoyote katika idadi kubwa ya watoto.

Utafiti huu pia unaonyesha ingawa walezi na walimu walitoa majibu sawa kuhusu hali ya ulemavu ya watoto fulani, majibu yao yalitofautiana kwenye vipengele maalumu vilivyosababisha changamoto. Walimu waligemea zaidi kwenye vipengele vinavyohusiana na masomo na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko, ilhali walezi walilenga hasa kwenye upungufu wa hisia, matatizo ya mawasiliano, changamoto za kupata marafiki na kuishi kwenye jamii, na afya ya kihisia. Utafiti huu unabaini kuwa utambuzi wa ulemavu huwa kwa njia mbalimbali na mitazamo tofauti ya walezi na walimu unaathiri utambuzi wao wa ulemavu.

**Licha ya kuwa walimu na walezi wanaweza kukubaliana juu ya uwepo wa ulemavu kwa mtoto, kuna uwezekano watafautiane kuhusu vipengeleo watavyozingatia haswa kulingana na majukumu yao kwa huyo mtoto, uzoefu, na yale yatayokuwa muhimu kwao.**

## Matokeo ya Walimu yakilinganishwa na yale ya wanafunzi:

Matokeo ya wanafunzi kwa maswali waliyoyajibu wenyewe kuhusu ugumu wa utendaji wao ulikuwa tofauti katika vipengele huku matokeo ya kipengele vya ukumbuzi yalikuwa ya juu Zaidi. Kulikuwa na kutokubaliana kwa matokeo ya wanafunzi na walimu ya kutathmini hali za ulemavu.

Kwa ufupi, utafiti unaonyesha kwamba walimu wanaweza kuzalisha takwimu thabiti za ulemavu yenye uaminifu wa kutosha kama wawakilishi. Matokeo yanaonyesha pia kuwa uthabiti wa matokeo ya mtafiti mmoja kati ya tathmini za walimu ulikuwa wa wastani. Hata hivyo, uthabiti wa matokeo ya walimu na yale ya walezi au watoto ulikuwa mdogo. Hii inatokana na tofauti za maoni, mitazamo, na vipaumbele kati ya watoa taarifa (walimu, walezi, na watoto).

### (3) Vigezo vya nje vinavyoathiri uthabiti wa matokeo vikiwemo idadi ya watoto darasani na ratiba ya tathmini

Kwa ujumla, walimu walijimudu sana katika kutathmini wanafunzi, hata kwenye madarasa yaliyo na idadi yakupindukia ya wanafunzi. Hata hivyo, kulikuwa na uwezekano kuwa majibu yalikisiwa wakati wahojiwa hawakuwa na uhakika. Utafiti ulibaini kwamba mahusiano kati ya walimu na wanafunzi yaliendelea kuwa bora kwa muda kadri walipoendelea kutumia CFM-TV.

Hata hivyo, ikiwa kipindi kuanzia mwanzo wa mwaka wa shule na tathmini ni muhimu (angalau mwezi mmoja au zaidi), si lazima kusubiri muda mrefu zaidi, kwani walimu walioshiriki katika utafiti huu waliweza kutathmini kila mwanafunzi katika darasa lao baada ya wiki chache.

### (4) Mabadiliko katika mienendo na shughuli za Maisha/ualimu

Matumizi ya CFM-TV na matokeo yake yameleta manufaa ambayo hayakutarajiwa katika elimu jumuishi yakiwemo walimu kubadilisha mitazamo na shughuli zao za ualimu. Pia mitazamo na kushiriki kwa wanafunzi kumeboreshwa. Utafiti huu ulionyesha mabadiliko tajika na muhimu katika mitazamo na tabia za walimu kwa kipindi cha muda mfupi.

**“Maswali haya yalinifanya nijhoji mwenyewe kwa maswala mengi. Kwa mfano, nilifunzaje mwanafunzi darasani mwangu, mwaka mzima bila kujua majina yake?” – mwalimu wa kiume, Tafiti za Kesi.**

**“Nahisi kama wanafunzi wangu sasa wanaona darasa letu kuwa kama lao wote. Mbeleni, ~wangesema ‘darasa langu’ lakini sasa ni ‘darasa letu’.” – mwalimu wa kike, Majadiliano ya Kikundi.**

Mafunzo ya siku mbili kwa walimu yaliyolenga kuongeza ufahamu na kueleza matumizi ya CFM-TV yalichangia sana kuzua manufaa. Pia walimu waliendelea kupata uhamasisho walipo kuwa wakikusanya takwimu hivyo kuendeleza manufaa. Matokeo ya ripoti hii yanasisitiza kwamba kukusanya data kuhusu ulemavu wa wanafunzi wakiwa shuleni ni muhimu kwasababu kunachangia kuboresha mazingira ya shule, mbinu za ufundishaji na shughuli za kusoma. Aidha, takwimu hizi zinachangia sana katika utunzi wa sera za elimu, kutenga rasilimali, na ufuatilizi wa matokeo ya shughuli na miradi. Kwa mtazamo wa kuendeleza maendeleo, takwimu hizi ni muhimu sana katika kupanga na kutathmini miradi.

## E. Hitimisho

**Matokeo ya utafiti huu yanazua mambo kadhaa muhimu yafuatayo:**

- **Kusuluhuhisha Pengo la Takwimu za Ulemavu:** Utafiti huu unasisitiza umuhimu wa kushughulikia ukosefu wa takwimu za ulemavu, hususan kuhusu watoto na vijana walio na ulemavu. Ukosefu huu wa takwimu rasmi kuhusu watoto walio na ulemavu hufanya watoto walio na ulemavu "wasioonekana kisiasa na kijamii," hali ambayo utafiti huu unalenga kuisahihisha.
- **Nafasi ya CFM-TV katika elimu:** CFM-TV inawezesha walimu kutathmini ugumu au utatizwaji wa utendaji wa wanafunzi wao darasani. CFM-TV inapeana nafasi na njia ya walimu kutathmini uwezo na changamoto za wanafunzi wao kwa kina, huku ikisuluhusha pengo kubwa katika ukusanyaji wa takwimu za ulemavu, hasa katika hali za dharura na migogoro ya muda mrefu.
- **Uthabiti na Manufaa ya CFM-TV darasani:** Matokeo yanaashiria kiwango cha uwiano wastani kati ya tathmini mbili zilizofanywa na walimu kila baada ya muda wa wiki tatu. Hata hivyo, inaonyesha jinsi walimu wanavyoweza kutumia maswali ya CFM-TV vilivyo ili kutathmini wanafunzi, hivyo kuchangia ukusanyaji wa takwimu sahihi. Ukubwa wa idadi ya watoto darasani haikuonekana kuathiri uwezo (na motisha) wa walimu kutathmini wanafunzi wote. Zaidi ya hayo, CFM-TV inaonyesha manufaa halisi, kama kuboresha mitazamo na mazoea ya walimu, pamoja na manufaa ambayo hayakutarajiwa katika tabia na ushiriki wa wanafunzi.
- **Walimu kama Wawakilishi:** Walimu na walezi wanaweza kuwa wawakilishi wa kutathmini hali ya ulemavu ya watoto, lakini takwimu zinazozalishwa hazitawiana na hazitalenga madhumuni yanayofanana.
- **Elimu Jumuishi katika Muktadha Mgumu:** Katika muktadha wa dharura na migogoro ya muda mrefu, utekelezaji wa elimu jumuishi hukumbana na changamoto kubwa. Ripoti hii ya utafiti inasisitiza kuwa kuna uwezekano wa CFM-TV kuwa na nguvu katika kuimarisha jitihada za elimu jumuishi katika muktadha wa dharura na migogoro ya muda mrefu. CFM-TV inachangia kufanikisha haki ya elimu bora kwa wote, pamoja na wale walio na ulemavu kwa kutoa njia kwa walimu kutambua na kushughulikia ugumu wa utendaji wa wanafunzi wao,

Hitimisho, ripoti hii ya utafiti inatetea umuhimu watakwimu sahihi katika kuelewa na kushughulikia mahitaji ya watoto na vijana walio na ulemavu, hususani katika mazingira magumu kama dharura na migogoro ya muda mrefu. Ripoti hii pia inaelekeza na kuashiria nyenzo Zaidi za utafiti zinazohitajika. Hata hivyo, CFM-TV ni suluhisho tendezi, inayotoa matokeo thabiti yanayofaa walimu pamoja na wanafunzi. Kwa kusuluhisha pengo la takwimu za ulemavu, CFM-TV inachangia kufikia lengo kubwa la elimu jumuishi, na kuhakikisha hakuna mtoto yeyote anaachwa nyuma, bila kujali uwezo wao au changamoto zao.



**Ripoti nzima ya utafiti inapatikana hapa:**
**www.hi.org/en/disability-data-in-schools-in-emergency-and-protracted-crisis**